

MAMLAKA YA USIMAMIZI WA WANYAMAPORI TANZANIA



TAARIFA KWA UMMA

UDHIBITI WA WANYAMAPORI WAKALI NA WAHARIBIFU KATIKA WILAYA YA MVOMERO

Morogoro,
15 Januari, 2023

Hivi karibuni kumesambaa picha jongefu "video" katika mtandao wa kijamii wa *Whatsapp* iliyomhusisha Mbunge wa Jimbo la Mvomero Mhe. Jonas Van Zeeland akizungumzia suala la uwepo wa tembo katika eneo la Lubungo Wilaya ya Mvomero.

Kipande cha video hiko kilirekodiwa katika Mkutano wa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mhe. Juma Hamidu Aweso (Mb) kilichofanyika katika Kijiji cha Lubungo Wilaya ya Mvomero tarehe 04/01/2023. Pamoja na kutoa maoni yake Mhe. Mbunge alitoa shutuma kwa askari wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) kutofanya kazi ya kudhibiti tembo waharibifu katika Wilaya ya Mvomero.

TAWA imechukulia maoni hayo kwa uzito mkubwa kwa kuzingatia kwamba yametolewa na muwakilishi wa wananchi. Hivyo, tunaomba kutoa ufafanuzi wa jambo hilo kama ifuatavyo;

Mosi, Kazi ya udhibiti wa wanyamapori wakali na waharibifu inatekelezwa kwa kuzingatia Mkakati wa kitaifa wa kutatua migongano baina ya binadamu na wanyamapori wa mwaka 2020 - 2024. Mkakati huo unaelekeza wadau mbalimbali kushirikiana katika udhibiti wa wanyamapori wakali na waharibifu. Kwa muktadha huo, udhibiti wa wanyamapori wakali na waharibifu katika Wilaya ya Mvomero siyo jukumu la TAWA pekee bali inatekelezwa kwa ushirikiano na Taasisi zingine za uhifadhi ikiwemo Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) kupitia Hifadhi ya Taifa Mikumi, Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI), Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero na Wananchi wote kwa ujumla.

Pili, TAWA kwa kushirikiana na TANAPA na Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero maeneo ya kiutendaji yaligawanywa ili kutoa huduma kwa wakati kwa wananchi katika Wilaya ya Mvomero. TAWA ilipewa kata sita (6) (Lubungo, Melela, Wami Dakawa, Mlali, Mzumbe, Homboza na Songaji). Hifadhi ya Taifa Mikumi ilipewa kata tatu (3) (Doma, Msongozi na Mangae). Aidha, Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Mvomero alitoa askari wanyamapori ili kushirikiana na askari wahifadhi katika kudhibiti wanyamapori waharibifu hususan tembo.

Aidha katika kukabiliana na changamoto katika Wilaya ya Mvomero kwa kipindi cha Oktoba 2020 hadi Desemba 2022 TAWA imefanya jitihada mbalimbali kama ifuatavyo: -

Mosi, Kufanya doria za kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu ambapo jumla ya siku-watu **3,284** za doria za kudhibiti matukio hayo zilifanyika dhidi ya matukio **264** yaliyo tolewa taarifa katika Wilaya ya Mvomero ikiwemo Kata ya Lubungo na Tarafa ya Mlali.

Pili, Takriban watu **4,151** walipewa elimu ya namna bora ya kuepuka madhara yanayosababishwa na wanyamapori wakali na waharibifu hususan tembo.

Tatu, TAWA imejenga kituo cha askari wa kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu kikiwa na pikipiki 4 na gari moja katika Kijiji cha Sangasanga kwa ajili ya Askari kufika kwa haraka kwenye matukio kabla tembo hawajaleta madhara.

Nne, Kufuatia uwepo wa matukio katika Kata ya Lubungo, tembo wanne (04) hatarishi walivunwa katika Kijiji cha Lubungo ambapo tembo wawili (02) mwaka 2021 na wengine wawili (02) mwaka 2022.

Tano, Kusambaza namba za kupiga simu bure (**0800110093**) ili kuripoti matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu inayotumika katika Mkoa wa Morogoro. Ambapo kupitia namba hiyo katika kipindi cha mwezi Julai hadi Desemba, 2022 **miito 48** ya matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu ilipokelewa na kufanyiwa kazi.

TAWA itaendelea kuwa mstari wa mbele katika kuimarisha ulinzi wa maisha ya watu na mali zao kwa kuchukua hatua stahiki ili kupunguza migongano baina ya binadamu na wanyamapori katika vijiji vya Wilaya ya Mvomero na maeneo mengine nchini. Tunaomba viongozi wa Serikali, wanasiasa na wananchi kwa ujumla kuunga mkono jitihada zinazofanyika na Mamlaka ipo tayari kupokea maoni na ushauri wa kuboresha na kuwatia moyo askari wazalendo wanaokesha mashambani siku zote kufukuza wanyamapori waharibifu hususan tembo.

Vilevile, TAWA inatoa rai kwa wananchi kupiga simu za dharura za kuripoti matukio haya na kuacha kuwachokoza au kuwapiga wanyamapori pale wanapowaona katika makazi yao ili kuepuka madhara zaidi kwa wananchi.

Imetolewa Na:



Vicky Kamata

Afisa Mhifadhi Mkuu-Uhusiano kwa Umma (TAWA)